



**TAMKO KULAANI KAULI ZINAZOHIMIZA KUUWAWA KWA
WANAOTETEA HAKI ZA KIJAMII**

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania umesikitishwa na unalaani vikali kauli mbalimbali zilizotolewa hivi karibuni na baadhi ya viongozi mbalimbali wa kisiasa zinazohimiza watu kuuliwa. Kauli hizo zimetolewa ndani na nje ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufuatia watetezi wa haki za binadamu na wanaharakati wa kisiasa akiwemo Mhe. Zuberi Zito Kabwe kuhimiza ulinzi wa haki ya mtoto wa kike kupata elimu nchini baada ya kujifungua.

Ibara ya 14 ya Katiba inasema wazi kwamba Kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka kwa jamii hifadhi ya maisha yake, kwa mujibu wa sheria. Haki ya kuishi haitolewi au sio zawadi kutoka kwa mtu yeyote bali ni haki ambayo mtu anazaliwa nayo na hakuna binadamu mwenye mamlaka ya kuondoa uhai wa mtu mwingine. Haki ya kuishi inalindwa pia na mikataba mbalimbali ya kimataifa ambayo Tanzania imeridhia. Kauli zinazohimiza kuuwawa kwa wataanzania wenzetu wanaojitokeza kutetea haki za makundi mbalimbali za kijamii ni za kupingwa na kila Mtanzania mzalendo na mpenda Amani na haki.

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania tunahimiza serikali kuchukua hatua dhidi ya wale wanaohimiza machafuko na visasi katika Taifa letu hili tulivu. Tunavishauri vyombo vya ulinzi na usalama kuwaita na kuwachukulia hatua stahiki wale wote waliojitokeza na kutoa matamshi hatarishi kwa Amani ya Taifa. Pia tunawaomba watetezi wote wa haki, viongozi wa dini, viongozi wa serikali na vyama kujitokeza na kukemea kauli hizi hatarishi kwa mustakabali wa Taifa. Endapo kuna mtu anaonekana kavunja sheria tuiachie vyombo vya haki vimuwajibishe na si kuanza kuhimiza watu kujichukulia sharia mikononi.

Imetolewa na

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania

03 Februari 2020

Board of Directors:

Ms. Vicky Ntetema, Michael Kyande, Kenneth Simbaya, Deogratius Nsokolo, Maxence Melo, Christina Kamili, Jamila M. Juma, Hassan Kh. Juma, Edwin Soko.